TANGAZO LA SERIKALI Na. 1011 la tarehe. 6/12/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO YA AFYA, USAFI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"afya" maana yake ni hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinachoweza kuliwa au kunyweka na binadamu isipokuwa dawa, na inajumuisha-

(a) Kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula;
(b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula; au
(c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula kama binzari na vingine vinavyofanana na hivyo;

"chanzo cha maji" maana yake ni eneo lolote ambalo limetengwa kwa ajili ya kuwa chanzo cha maji kwa matumizi ya jamii ikiwemo visima, mito,

chemchemi, vijito na maeneo yote yanapopatikana maji;

"choo bora" maana yake ni choo chochote cha maji chenye sakafu inayosafishika, banda imara la kudumu, lililoezekwa, lenye mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu;

"eneo la utalii" maana yake ni maeneo ya vivutio yaliyopo katika eneo la Halmashauri ikiwemo na fukwe za bahari;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji;

"jengo la biashara" maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya biashara iliyokusudiwa;

"kaya" maana yake ni baba, mama na mtoto au watoto au mtu yeyote aliyetimiza umri wa miaka kumi na nane anayeishi kwa kujitegemea;

"kero" au "chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa au ni kichafu kiasi cha kusababisha-

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu;
(b) harufu mbaya au harufu ya kuudhi au kuleta kinyaa; au
(c) kuzaliana kwa wadudu hatari kama vile nzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;

"kuchakata taka" maana yake ni kuchambua, kutenganisha na kubadili taka kuwa kitu kingine chenye manufaa kwa jamii;

"magonjwa ya mlipuko" maana yake ni magonjwa yanayotokea kwa muda mfupi ya kuambukiza na kuenea kwa haraka na kuathiri watu wengi ndani ya muda mfupi yanayoweza kutolewa amri ya

tahadhari, kupooza, kipindupindu, kuhara, surua na homa ya matumbo;

Sura ya 191

"maji" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191

"maji taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191

"mazingira" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mifugo" maana yake ng'ombe, punda, nguruwe, mbuzi, mbwa, kondoo au kuku na wanyama wengine wote wafugwao majumbani;

Sura ya 323

"misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

"pipa la taka" maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira;

Sura ya 191

"taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191

"taka ngumu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191

"taka za viwandani" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na wajibu wa:

(a) kusimamia utekelezaji wa shughuli za afya, usafi na usimamizi wa mazingira;

(b) kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kufuata kanuni za afya, usafi na kutunza mazingira;

(c) kuteua Wakala kutekeleza shughuli za usimamizi wa afya, usafi na mazingira kwa niaba ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) kufanya ukaguzi ili kubaini endapo kanuni za afya, usafi na utunzaji wa mazingira zinazingatiwa ndani ya eneo la Halmashauri;

(e) kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote anayekiuka Sheria Ndogo hii au sheria nyingine inayohusiana na afya, usafi na usimamizi wa mazingira zilizotungwa na Bunge; na

(f) kutengeneza kanuni , miongozo au kutoa maelekezo yatakayosaidia kulinda afya, usafi na usimamizi wa mazingira ndani ya eneo la Halmashauri;

Upimaji wa afya

5. Itakuwa ni wajibu kwa mtu yeyote anayejishughulisha na biashara au huduma ya chakula kupima afya kila baada ya miezi sita.

Usafi wa mazingira

6. Mtu yeyote anayemiliki au kutumia jengo au eneo ambalo halijaendelezwa au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba:

(a) majani yanayozunguka jengo lake au makazi yanakatwa au kupaliliwa na kuondolewa katika eneo lake lote;

(b) taka ngumu zote ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki zitakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;

(c) maji taka yanaelekezwa ndani ya mfumo wa maji taka;

(d) kuboresha na kupaka rangi jengo lake kila linapochakaa;

(e) anakuwa na choo bora;

(f) atashiriki siku ya usafi ya jumamosi ya kila mwisho wa mwezi;

(g) anaondoa uchafu ikiwemo mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo katika

mfereji wa maji ya mvua inayomzunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mifereji hiyo inakuwa safi wakati wote;

(h) hakuna mkusanyiko wa maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuathiri upitishaji wa maji ya mvua na hivyo kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla;

(i) anafanya uchambuzi wa taka;

(j) kuna chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhia taka ngumu kabla hazijachukuliwa kwa ajili ya kwenda kutupwa katika eneo lilotengwa kwa ajili ya kuhifadhi taka;

(k) anatunza na kuhifadhi vyombo vya kuhifadhia taka vinavyowekwa na Halmashauri; na

(l) kuna chombo maalumu cha kuhifadhia maganda ya matunda, madafu, miwa, maembe, mafenesi au mabaki ya matunda.

Kutiririsha maji taka

7.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kutiririsha au kumwaga au kutapisha au kuruhusu au kusababisha kutiririsha au kumwaga au kutapisha maji taka barabarani, uchochoroni, kwenye mifereji, mtoni, kwenye vyanzo vya maji au sehemu yoyote isiyotengwa kwa ajili ya kuhifadhi maji taka.

(2) Kila kiwanda kinachozalisha maji taka kitakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa kinaunganisha maji taka au kujenga mifereji na mabwabwa kwa ajili ya kuhifadhi maji taka.

(3) Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo la kuhifadhi linapojaa na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha karo kujaa na kutiririsha au kutapisha maji taka barabarani au sehemu yoyote isiyoruhusiwa.

Utengenezaji na uuzaji vyakula

8. Mfanyabiashara yeyote wa chakula hataruhusiwa kutengeneza, kuchoma, kupika,

kuchemsha na kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote au kwenye nyumba yoyote isipokuwa kama ametimiza masharti na kanuni za afya.

Uuzaji wa vyakula vilivyopikwa

9.-(1) Mtu yeyote anayeendesha biashara ya vyakula vya kupika au kukaanga atakuwa na wajibu wa kuhakikisha vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku safi lililowekwa kioo ili kuzuia nzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote-

(a) kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini, vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza; na

(b) kupanga vyakula nje ya duka la vyakula.

Usalama wa matumizi ya maji

10.-(1) Kila mkazi anapaswa kuhakikisha kwamba maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama bila kujali yanatoka kwenye chanzo gani cha maji.

(2) Kila mmiliki wa kisima atapaswa kuhakikisha maji ya kisima yamepimwa ili yawe salama kwa matumizi ya binadamu.

Uzuiaji wa shughuli wakati wa magonjwa ya mlipuko

11. Mkurugenzi anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

Ukamataji wakati wa zuio

12.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kumkamata mtu yeyote ambaye atakaidi amri ya zuio la kufanya shughuli ya uuzaji wa vyakula wakati wa magonjwa ya mlipuko.

(2) Endapo mtu aliyekamatwa alikuwa anauza vyakula ambavyo vinaharibika kwa haraka, Halmashauri itaharibu vyakula hivyo.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2), endapo vyakula vilivyokamatwa vitakuwa haviharibiki kwa haraka, Halmashauri itakuwa na jukumu la kuvihifadhi hadi mwisho wa amri ya zuio.

(4) Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokana na ukamataji na uharibifu, isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa Afisa wa Halmashauri au wakala wake.

Udhibiti wa ubebaji kokoto, mawe na mchanga

13. Mtu yeyote atakayesafirisha mawe, mchanga au kokoto katika eneo la Halmashauri atahakikisha kuwa chombo anachotumia kusafirisha kimefunikwa ili kuzuia kumwagika na kuchafua mazingira.

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

14.-(1) Kila mmiliki wa nyumba atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba:

(a) nyumba yake ina choo safi, imara kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo;

(b) anaweka sehemu maalum ya kunawia mikono ikiwa na maji safi na sabuni maalum ya kimiminika.

(2) Choo kitajengwa umbali wa mita sitini kutoka chanzo chochote cha maji.

Vyoo vya umma

15. Halmashauri inaweza kujenga choo cha umma au kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona inafaa na vitatakiwe view vya kudumu na viwe na-

(a) matundu yasiyopungua mawili kwa wanawake na mawili kwa wanaume;

(b) mfumo madhubuti wa maji na uwepo wa maji ya kutosha yaliyo safi na salama;

(c) kuwepo na chombo cha kuhifadhia maji ya akiba;

(d) kuwepo kwa bafu ya wanaume na wanawake;

(e) kuwepo na chumba maalumu cha kuvutia sigara;

(f) kuwepo na sehemu ya haja ndogo kwa wanaume; na

(g). kuwepo na chombo maalumu chenye mfuniko cha kuhifadhia taka zisizoweza kusukumwa na maji.

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

16. Mtu yeyote, kikundi au taasisi yenye lengo la kukusanya watu kwa madhumuni ya mkutano au sherehe au mkusanyiko wowote kuweka au kujenga vyoo vya muda endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu baada ya kuomba kibali kutoka Halmashauri.

Vyoo katika majengo ya biashara

17. Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hii kwa ajili ya matumizi ya wateja wake kwa kuzingatia jinsia zote.

Ilani ya kujenga au kurekebisha choo

18. Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Ilani ya kuondoa kero

19.-(1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ndani ya siku saba kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

Udhibiti utupaji wa taka

20.-(1) Wamiliki wa vyombo vya usafiri vya umma watalazimika kuweka vyombo vya kuhifadhia taka ili abiria wasitupe taka nje vyombo vya usafiri.

(2) Wamiliki wa vyombo vya usafiri vya binafsi watahakikisha kuwa wenyewe au watu waliomo katika vyombo vyao hawatupi taka nje ya vyombo hivyo vya usafiri.

(3) Mtu yeyote hataruhusiwa kutupa taka ovyo katika maeneo ya makazi, biashara, mifereji ya maji ya mvua, hifadhi ya barabara au mahali popote pasipotengwa kwa ajili ya kutupa taka.

(4) Mtu yeyote au mkazi atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba anatupa uchafu au taka katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalum yaliyotengwa.

Ukusanyaji Taka ngumu

21.-(1) Halmashauri itawajibika kukusanya taka ngumu kutoka katika maeneo ya kutunza taka kwa muda ulioainishwa katika kila Kata.

(2) Taka ngumu zote zitakazokusanywa kwenye mapipa ya taka zitabaki kuwa mali ya mkazi au mmliki wa eneo lile mpaka zitakapokuwa zimefikishwa kwenye maeneo ya kutunza taka kwa muda au zitakapokuwa zimetolewa na Wakala kutoka katika eneo lake.

(3) Haitaruhusiwa kuweka uchafu wenye asili ya maji maji kwenye pipa la taka au kitu chochote kinachoweza kulipuka na kusababisha madhara.

Ada ya uzoaji taka

22.-(1) Kutakuwa na ada ya uzoaji taka ambayo itatozwa na Halmashauri kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa mazingira kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(2) Ada ya uzoaji taka itatozwa kwa viwango tofauti kulingana na vipato na maeneo mbalimbali ya makazi kama yalivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

(3) Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Eneo la kutupa taka

23.-(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kutenga, kuanzisha, kujenga na kuendesha maeneo makuu ya kutupa taka na maeneo ya kutunza taka kwa muda;

(b) kuanzisha na kusimamia vituo vya kukusanya taka na kuweka utaratibu wa uendeshaji; na

(c) kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji wa taka hadi kwenye dampo.

(2) Halmashauri itatoza gharama za utupaji taka kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

Taka hatarishi

24. Mtu yeyote, kampuni, wakala au taasisi haitaruhusiwa kuendesha shughuli za uchomaji wa taka hatarishi bila ya kupata ushauri kutoka Halmashauri.

Taka za viwanda

25.-(1) Kila mwenye kiwanda atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na taka nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe hai wengine.

(2) Kiwanda chochote hakitaruhusiwa kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya, vumbi au kelele na kusababisha kero kwa wakazi.

Uhifadhi wa maji taka

26. Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda au eneo la biashara anatakiwa-

(a) kuhakikisha kuwa analo karo la kuhifadhi maji taka;
(b) kunyonya maji taka pale karo linapojaa;
(c) kutotiririsha, kutotapisha au kutoelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni au viwandani kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhia maji taka; na
(d) kuhakikisha kuwa anaunganisha maji taka au kujenga mifereji na mabwabwa kwa ajili ya kuhifadhi maji taka.

Uchambuzi wa taka

27.-(1) Taka zote zitachambuliwa kwa makundi ya taka kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(2) Taka zote zitapaswa kuchambuliwa sehemu zinakotoka katika makundi ya taka zenye madhara na zisizo na madhara ili kuwezesha utofauti katika usimamizi, usafirishaji na utupaji wake.

(3) Taka zote zilizo na madhara zitatunzwa kwenye chombo cha rangi nyekundu kilichowekewa alama ya "Taka hatarishi".

(4) Taka zote zenye ncha kali zitatunzwa au kuwekwa kwenye mifuko ya pekee na kuwekwa alama ya kutoa tahadhari inayosema "Hatari usifungue".

(5) Taka zote zinazohusiana na taka rejea zitachambuliwa na kuwekwa kwenye vyombo maalum vitakavyoelekezwa na Afisa Mwidhiniwa.

Uanzishwaji wa Vikundi Jamii

28. Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa vikundi jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji na eneo la hifadhi

29.-(1) Halmashauri itawajibika kusimamia, kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kulima au kukata miti au kuchunga mifugo katika umbali wa mita sitini kutoka chanzo cha maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(3) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

(4) Halmashauri na jamii husika itakuwa ni wajibu wa kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya wataalam.

(5) Mtu yeyote hataruhusiwa kumiliki eneo la chanzo cha maji.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

30. Mtu hataruhusiwa -

(a) kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai;

(b) kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai; au

(c) kuunganisha maji ya mvua na maji taka au kutapisha choo na kutiririsha vinyesi vya mifugo au binadamu kwenye chanzo cha maji au mfereji wa maji ya mvua.

Kuchoma au kusababisha moto

31.- (1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuchoma au kusababisha moto katika misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(2) Ni wajibu wa kila mwananchi kuzima moto ambao utaonekana kuwaka katika eneo la Halmashauri yenye kuleta viashiria vya hatari.

Uvunaji miti

32.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote-

(a) kukata miti katika eneo la Halmashauri kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri; au

(b) kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalum ambao ni rasilimali ya Taifa.

(2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Mtu anaetaka kuvuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa, mbao au kuni atatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kazi hiyo na atatakiwa kulipa ada ijulikanayo kama ada ya uchafuzi wa mazingira kwa kiwango kilichoainishwa kwenye Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kupanda miti

33. Kila mmiliki wa jengo la makazi au biashara atawajibika kutunza na kupanda miti katika eneo lake kama inavyofafanuliwa katika Jedwali la Sita la Sheria Ndogo hii.

Tathimini ya athari kwa mazingira

34.-(1) Miradi yote inayotekelezwa ndani ya Halmashauri haitaendelezwa bila kufanyiwa tathmini ya athari ya mazingira.

(2) Kila mpendekezaji wa mradi atawajibika kulipa Halmashauri asilimia kumi ya gharama ya tathmini ya athari ya mazingira kama ada ya ukaguzi na usimamizi wa mradi husika.

Uhifadhi wa mazingira ya bahari na udhibiti wa rasilimali zake

35. Mtu hataruhusiwa-

(a) kutumia uvuvi wa juva, baruti, sumu au mkuki;
(b) uvulia nyavu kwenye maji mafupi au kwenye miamba;
(c) kuvua, kuokota, kuchukua au kufanya kitendo chochote kwenye maeneo tengefu ya samaki isipokuwa kwa kibali maalum cha Halmashauri;
(d) kuvua samaki bila kuwa na leseni ya uvuvi; au
(e) kutumia chombo cha uvuvi kisichokuwa na namba za usajili pamoja na leseni ya chombo hicho.

Usimamizi wa vivutio vya utalii vya Halmashauri

36. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kusimamia, kuboresha na kuendesha vituo vya utalii inavyovimiliki vilivyopo katika eneo la Halmashauri.

Kibali cha kutumia eneo la utalii

37.-(1) Mtu yeyote anayetaka kutumia eneo la utalii atatakiwa kuomba kibali kutoka Halmashauri kwa kuwasilisha barua ya maombi kwa Mkurugenzi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Saba la Sheria Ndogo hii.

(2) Kibali hicho kitatolewa kwa mwombaji kupitia Afisa Mwidhiniwa na mwombaji atalipia ada ya kibali cha kutumia eneo la utalii.

(3) Kibali kitakachotolewa kitajumuisha masuala yafuatayo:

(a) kupasua magogo yaliyolala chini;
(b) kufanya utafiti ndani ya msitu;

(c) kuweka kambi ndani ya msitu;
(d) kufanya ziara ya mafunzo ndani ya msitu;
(e) kutundika mizinga ya nyuki;
(f) kukagua na kurina asali;
(g) kutafuta dawa za asili bila kudhuru viumbepori;
(h) kufanya matambiko; na
(i) kuchuma matunda, mboga za majani na uyoga.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (2) Afisa Mwidhiniwa anaweza kutoa kibali kwa masuala mengine kwa kadri atakavyoona inafaa.

Kufuta kibali

38.-(1) Afisa Mwidhiniwa anaweza kufuta kibali cha kutumia eneo la utalii endapo mmiliki kibali hicho atakitumia kinyume na masharti yaliyowekwa.

Ada za kutumia eneo la utalii

39. Halmshauri itatoza ada ya kutumia maeneo ya utalii kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika katika Jedwali la Nane la Sheria Ndogo hii.

Uteuzi wa Wakala

40.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Wakala wa kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala atakayeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hii atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya kwa niaba ya Halmashauri, ada au ushuru mbalimbali zinazohusiana na afya, usafi na usimamizi wa mazingira katika eneo lake alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hii;
(b) kutumia mfumo wa kielektroniki katika kukusanya ada au ushuru na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri; na
(c) kuzingatia masharti ya mkataba wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Makosa

41. Mtu ambaye-

(a) atatupa taka au uchafu wowote au kuacha takataka au uchafu kwenye nyumba, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au eneo linalopakana na nyumba yoyote au ardhi yoyote au karibu na maeneo ya nyumba au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo.
(b) atamzuia au kujaribu kumzuia au atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii;
(c) atamwaga taka barabarani, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni, au mahali popote hadharani au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;
(d) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;
(e) atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;
(f) atapika vyakula pembezoni mwa barabara au nje ya majengo mengine;
(g) atauza vyakula maeneo yasiyo rasmi na kushindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;
(h) ataacha nyumba anayoishi au kumiliki au kufanyia shughuli zake katika hali ya uchafu yenye kuleta kero au chukizo;

(i) ataacha chombo cha usafiri katika hali ya uchafu;
(j) ataendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;
(k) ataenda haja ndogo au kubwa hovyo barabarani, uchochoroni, upenuni;

(l) atafanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo;

(m) atafanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(n) ataendesha gari linalosababisha uchafuzi wa mazingira kwa kutoa moshi mzito unaoonekana;

(o) atavua samaki kwa kutumia sumu au nyavu zenye matundu madogo;

(p) ataharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji atakuwa;

(q) ataweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe hai wengine ambao ni rasilimali ya Taifa;

(r) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali;

(s) atabandua magome ya miti kwa ajili ya kutengeneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila ya kuwa na kibali;

(t) atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo; au

(u) ataruhusu mhudumu yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya yake,

anatenda kosa.

Adhabu

42. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa lolote kinyume cha Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki tatu na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

kufifilisha kosa

43. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Tisa la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa TS. Na. 526 la 2019, na TS.Na.602 la 2019 na TS.Na.31 la 2017.

44. Sheria Ndogo ya Afya na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ya mwaka 2019, na Sheria Ndogo ya Afya na Usimamizi wa Mazingira (Marekebisho) ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ya mwaka 2019; na Sheria Ndogo ya Udhibiti Taka na Utunzaji wa Mazingira ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2017 zinafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 18 na 19(1)*)

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM
ILANI YA KUREKEBISHA AU KUONDOA KERO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo ya Afya,Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Jiji La Dar es Salaam ya Mwaka 2024.

SEHEMU "A"

Ndugu .................................................... wa S.L.P ..................................unaarifiwa kwamba katika ukaguzi wa ....................................................... uliofanyika tarehe..............mwezi wa ...........................mwaka ......................... katika nyumba yako ya ................................... biashara au kuishi au kutolea huduma au kiwanja iliyopo eneo la .......................................... kumekutwa machukizo au kero au uchafu kama ifuatavyo:-

1)................................................................
2) ...............................................................
3) ................................................................

SEHEMU "B"

Kwa ilani hii unaamuriwa kurekebisha au kuondoa au kusafisha kwa:-

1)................................................................
2) ...............................................................
3) ................................................................

SEHEMU "C"

Unapewa muda wa siku .......... tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza yote yaliyoelezwa katika sehemu "B" ya ilani hii , kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kulazimika kukupa taarifa nyingine.

....................................................
JINA:
Afisa Muidhiniwa

| IMETOLEWA NA:- | IMEPOKELEWA NA:- |
|---|---|
| Jina: ............................ | Jina: ............................. |
| Sahihi: ....................... | Sahihi: .......................... |
| Wadhifa: ................... | Wadhifa: ....................... |
| Tarehe:...................... | Tarehe: ......................... |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 22(1)*

ADA YA UZOAJI WA TAKA

| Namba | Aina ya Makazi | Kipato cha juu kwa mwezi | Kipato cha Kati kwa mwezi | Kipato cha chini kwa mwezi |
|---|---|---|---|---|
| | NYUMBA | | | |
| 1 | Nyumba za ghorofa (Kwa kaya) | 15,000 | 7,000 | 3,000 |
| 2 | Nyumba za chini (kwa kaya) | 8,000 | 3,500 | 2,500 |
| 3 | Nyumba mpya za ghorofa usanifu wa kawaida | 15,000 | 7,000 | 3,000 |
| 4 | Nyumba mpya za ghorofa usanifu wa kisasa | 15,000 | 10,000 | 5,000 |
| 5 | Nyumba ya pekee | 25,000 | 20,000 | 10,000 |
| 6 | Nyumba ya pekee yenye nyumba za huduma (Villa) | 30,000 | 20,000 | 15,000 |

| Namba | Aina ya mzalishaji wa taka | Kiwango cha ada/ushuru kwa mwezi | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Kipato cha juu | Kipato cha kati | Kipato cha chini |
| 7 | Penthouse | 50,000 | 40,000 | 25,000 |
| 8 | Hostel (kwa mpangaji au mkazi) | 500 | 500 | 500 |
| 9 | Hostel (kwa chumba) | 2,000 | 2,000 | 2,000 |
| 10 | Nyumba ya kulala wageni | 40,000 | 30,000 | 20,000 |
| 11 | OFISI | | | |
| | • Ofisi yenye wafanyakazi 1 – 10 | 30,000 | 20,000 | 10,000 |
| | • Ofisi yenye wafanyakazi 11 – 50 | 60,000 | 60,000 | 40,000 |
| | • Ofisi yenye wafanyakazi 51 – 100 | 150,000 | 150,000 | 100,000 |
| | • Ofisi yenye wafanyakazi 101 na zaidi | 250,000 | 250,000 | 150,000 |
| | BENKI | | | |
| 12 | Tawi la Benki | 150,000 | 150,000 | 150,000 |

*Tangazo la serikali Na.1011 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 13 | Duka la kubadilishia fedha | 100,000 | 100,000 | 100,000 |
| 14 | Ofisi za ATM | 100,000 | 100,000 | 100,000 |
| 15 | Ofisi za luku (Tanesco) | 100,000 | 100,000 | 100,000 |
| 16 | Ofisi za luku (Wakala) | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| 17 | Ofisi za Mawakala wa fedha, luku (Tanesco), na mitandao ya simu | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| | VYAKULA NA VINYWAJI | | | |
| 18 | Sehemu ya kuuzia chai na vitafunwa | 20,000 | 15,000 | 10,000 |
| 19 | Mgahawa | 30,000 | 20,000 | 15,000 |
| 20 | Duka la vyakula na vinywaji | 20,000 | 15,000 | 10,000 |
| 21 | Baa (pombe, vinywaji baridi na vitafunwa) | 30,000 | 30,000 | 20,000 |
| 22 | Mama na baba lishe | 15,000 | 10,000 | 5,000 |
| 23 | Taka zinazotokana na Biashara ya Mgahawa wa nje ya Majengo | 10,000 | 60,000 | 20,000 |
| 24 | Vibanda vya chips | 15,000 | 10,000 | 5,000 |
| 25 | Baa na mgahawa au jiko | 50,000 | 30,000 | 20,000 |
| 26 | Baa na nyumba ya kulala wageni | 50,000 | 50,000 | 30,000 |
| 27 | Baa, nyumba ya wageni na ukumbi wa starehe | 100,000 | 60,000 | 40,000 |
| 28 | Baa na ukumbi wa starehe | 100,000 | 50,000 | 30,000 |
| 29 | Baa, ukumbi wa starehe na mgahawa | 100,000 | 50,000 | 30,000 |
| 30 | UKUMBI WA STAREHE | | | |
| | Watu 01 hadi 50 | 100,000 | 50,000 | 30,000 |
| | Watu 51 hadi 300 | 150,000 | 150,000 | 150,000 |
| | Watu 301 hadi750 | 300,000 | 300,000 | 300,000 |
| | Watu 751 hadi 2000 | 500,000 | 500,000 | 500,000 |
| | Watu 2001 na kuendelea | 1,000,000 | 1,000,000 | 1,000,000 |
| | Duka la kuuza Ice Cream | 20,000 | 10,000 | 10,000 |
| 31 | HOTELI | | | |
| | 10 Vyumba | 100,000 | 100,000 | 50,000 |
| | 11- 20 Vyumba | 200,000 | 200,000 | 150,000 |
| | 21- 30 Vyumba | 300,000 | 300,000 | 250,000 |
| | 31- 40 Vyumba | 400,000 | 400,000 | 300,000 |
| | 41- 50 Vyumba | 500,000 | 500,000 | 400,000 |
| | 51- 70 Vyumba | 600,000 | 600,000 | 500,000 |
| | 71- 100 Vyumba | 700,000 | 700,000 | 600,000 |
| | 101- Na kuendelea | 1,300,000 | 1,300,000 | 1,000,000 |
| 32 | BUCHA YA NYAMA NA SAMAKI | 10,000 | 5,000 | 5,000 |
| 33 | DUKA ( JUMLA NA REJA REJA) | | | |

*Tangazo la serikali Na.1011 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 34 | Vyakula au Bidhaa mchanganyiko | 30,000 | 15,000 | 10,000 |
| | Duka la Nguo | 20,000 | 10,000 | 5,000 |
| 35 | Vifaa vya umeme au simu | 40,000 | 30,000 | 20,000 |
| 36 | Vifaa vya ujenzi | 50,000 | 40,000 | 30,000 |
| 37 | Vitabu au Shajala | 20,000 | 10,000 | 5,000 |
| 38 | Urembo au Vipodozi | 40,000 | 30,000 | 20,000 |
| 39 | Duka la Samani | 40,000 | 30,000 | 20,000 |
| 40 | Vinywaji na Pombe Kali | 30,000 | 20,000 | 10,000 |
| 41 | Taka zinazotokana na ghala la kuhifadhia bidhaa | 30,000 | 20,000 | 10,000 |
| 42 | Vipuri na Vifaa vya magari | 20,000 | 10,000 | 10,000 |
| 43 | Duka la Vifaa vya muziki na kaseti | 40,000 | 30,000 | 20,000 |
| 44 | Duka la Vitu vya Chakula | 20,000 | 20,000 | 10,000 |
| 45 | Duka la baiskeli | 30,000 | 20,000 | 10,000 |
| 46 | Duka la pikipiki | 40,000 | 20,000 | 10,000 |
| 47 | Showrooms za magari | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| | KARAKANA | | | |
| 48 | Fundi Seremala | 30,000 | 20,000 | 10,000 |
| 49 | Karakana ya Chuma | 50,000 | 30,000 | 20,000 |
| 50 | Karakana ya Magari | 50,000 | 30,000 | 20,000 |
| 51 | Sonara na uhunzi wa vito | 15,000 | 10,000 | 5000 |
| 52 | Shughuli za Vioo au Shughuli za Alminium | 100,000 | 50,000 | 30,000 |
| 53 | Mchapishaji | 100,000 | 30,000 | 20,000 |
| 54 | Store | 40,000 | 30,000 | 20,000 |
| 55 | Mashine ya Mbao kwa ujazo wa mita moja | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| | VIWANDA VIDOGO NA VIKUBWA | | | |
| 56 | Taka kwa ujazo wa cubic mita | 45,000 | 25,000 | 25,000 |
| 57 | Matengenezo ya vifaa vya umeme | 45,000 | 15,000 | 10,000 |
| 58 | Matengenezo ya matairi | 40,000 | 15,000 | 10,000 |
| 59 | Magurudumu na Matengenezo | 100,000 | 50,000 | 30,000 |
| | BIASHARA NDOGO NA NYINGINEZO | | | |
| 60 | Fundi Cherehani | 20,000 | 10,000 | 5,000 |
| 61 | Seremala | 20,000 | 10,000 | 5,000 |
| 62 | Fundi viatu | 5,000 | 3,000 | 2,000 |
| 63 | Saluni ya Nywele | 20,000 | 10,000 | 5,000 |
| 64 | Dobi | 10,000 | 5,000 | 5,000 |
| 65 | Genge kwa meza moja | 5,000 | 3,000 | 2,000 |
| 66 | Biashara ya juisi ya miwa | 40,000 | 30,000 | 20,000 |
| | (a) Wauza matunda na juisi nyinginezo | 30,000 | 20,000 | 10,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (b) Wafanyabiashara wadogo wasio na maeneo maalum | ---------- | --------- | 500 kwa siku |
| 67 | Huduma za Internet | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| | HUDUMA ZA AFYA (TAKA ZISIZOKUWA ZA HATARI) | | | |
| 68 | Duka la dawa baridi | 30,000 | 20,000 | 10,000 |
| 69 | Duka la Dawa Rejareja | 50,000 | 40,000 | 30,000 |
| 70 | Duka la dawa la jumla | 100,000 | 70,000 | 50,000 |
| 71 | Duka la Vifaa vya Maabara | 40,000 | 30,000 | 20,000 |
| 72 | Maabara ya Vipimo | 20,000 | 10,000 | 5,000 |
| 73 | Zahanati | 50,000 | 30,000 | 15,000 |
| 74 | Kituo cha Afya | 20,000 | 10,000 | 5,000 |
| 75 | Vituo vya tiba mbadala au asilia | 50,000 | 30,000 | 15,000 |
| 76 | Duka la dawa asilia | 20,000 | 10,000 | 5,000 |
| 77 | Hospitali | 100,000 | 100,000 | 100,000 |
| 78 | Kliniki | 30,000 | 20,000 | 10,000 |
| 79 | Hospitali ya Rufaa | 400,000 | 400,000 | 400,000 |
| | TAASISI ZA MAFUNZO | | | |
| 80 | Kituo cha kulelea watoto, Shule ya Sekondari, Shule ya Msingi na Vyuo vya Kutwa | | | |
| | Wanafunzi 01-200 | 40,000 | 30,000 | 15,000 |
| | Wanafunzi 201- 500 | 80,000 | 50,000 | 30,000 |
| | Wanafunzi 501-1,000 | 150,000 | 100,000 | 80,000 |
| | Wanafunzi 1001 na kuendelea | 250,000 | 250,000 | 250,000 |
| 81 | Shule na Vyuo vya Bweni | | | |
| | Wanafunzi 01-200 | 60,000 | 60,000 | 60,000 |
| | Wanafunzi 201- 500 | 150,000 | 150,000 | 150,000 |
| | Wanafunzi 501-1,000 | 250,000 | 200,000 | 150,000 |
| | Wanafunzi 1001 na kuendelea | 400,000 | 300,000 | 300,000 |
| | VITUO VYA MAFUTA | | | |
| 82 | Kituo kikubwa cha Mafuta | 100,000 | 100,000 | 100,000 |
| 83 | Kituo kidogo cha Mafuta | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| 84 | Kituo cha Mafuta ya taa | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 85 | Kituo cha Kuuzia gesi | 20,000 | 15,000 | 10,000 |
| 86 | Kibanda cha Kuuzia mkaa | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| | HUDUMA NYINGINEZO | | | |
| 87 | Misikiti na Makanisa | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 88 | Nyumba ya Starehe au Klabu au cassino au night clubs | 250,000 | 100,000 | 50,000 |
| 89 | Ofisi za ulinzi | 20,000 | 10,000 | 5000 |
| 90 | Teksi kwa siku | 500 | 500 | 500 |

*Tangazo la serikali Na.1011 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 91 | Vituo vya kushusha na kupakia mizigo | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 92 | Minara ya simu | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| 93 | Taka za Bustani kwa Mita Mraba Moja | 25,000 | 25,000 | 25,000 |
| 94 | Taka za Masoko kwa cubic mita | 25,000 | 25,000 | 25,000 |
| 95 | Ghala | 100,000 | 100,000 | 100,000 |
| 96 | Bahati nasibu | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| 97 | Super Market | 300,000 | 300,000 | 300,000 |
| 98 | Mini SuperMarket | 100,000 | 100,000 | 100,000 |
| 99 | Taka za Uvunjaji wa Majengo kwa tani | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| 100 | Kituo cha Kuchakata Taka | 100,000 | 50,000 | 30,000 |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 22(2)*

MGAWANYO WA KATA KULINGANA NA KIPATO

| Namba | Kanda "A" –Kipato cha juu | Kanda "B"- Kipato cha Kati | Kanda "C"-Kipato cha Chini |
|---|---|---|---|
| 1. | Upanga Mashariki | Kinyerezi | Kipawa |
| 2. | Upanga Magharibi | Kimanga | Kiwalani |
| 3. | Kisutu | Mchikichini | Pugu |
| 4. | Mchafukoge | Segerea | Gongo la mboto |
| 5. | Gerezani | Ilala | Majohe |
| 6. | Kivukoni | Tabata | Kivule |
| 7. | Kariakoo | Jangwani | Ukonga |
| 8. | | | Kitunda |
| 9. | | | Chanika |
| 10. | | | Msongola |
| 11. | | | Vingunguti |
| 12. | | | Bonyokwa |
| 13. | | | Buyuni |
| 14. | | | Kipunguni |
| 15. | | | Kisukuru |
| 16. | | | Liwiti |
| 17. | | | Minazi Mirefu |
| 18. | | | Mnyamani |
| 19. | | | Pugu station |
| 20. | | | Zingiziwa |
| 21. | | | Mzinga |
| 22. | | | Buguruni |
| | | | |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 23 (2))*

GHARAMA ZA UTUPAJI TAKA

| Namba | Chanzo | Ujazo/kipimo | Kiwango cha ada shilingi |
|---|---|---|---|
| 1. | Taka za majumbani zisizochambuliwa | Tani | 5,000/= |
| 2. | Taka za majumbani zilizochambuliwa | Tani | 3,000/= |
| 3. | Taka za Viwandani na sehemu za biashara | Tani | 18,500/= |
| 4. | Kuharibu mali zilizokwisha muda wa matumizi. | Tani | 100,000/= |
| | | Chini ya tani Moja | 90,000/= |
| 5. | Taka zenye madhara isiyo madawa | Kilo | 1,000/= |
| 6. | Taka ya madawa (Red/Blue bag) | Kilo | 4,000/= |
| 7. | Taka za madawa yenye ncha kali na gesi (bio-medical) | Kilo | 5,000/= |
| 8. | Taka za madawa- Vimiminika | Lita | 2,000/= |
| 9. | Taka za magurudumu ya magari baiskeli, piki piki | Kilo | 1,000/= |
| 10. | Taka zinginezo | Tani | 50,000/= |
| 11. | Kibali cha magari ya kusafirisha taka | Gari | 200,000/= |

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 32(3)*

ADA YA UCHAFUZI WA MAZINGIRA

| Namba | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mkaa | 1,000 kwa gunia |
| 2. | Mbao | 5,000 kwa kila ujazo wa mita moja |
| 3. | Kuni | kwa kila ujazo wa mita moja |

JEDWALI LA SITA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 33)*

UPANDAJI MITI

| Namba | Aina ya Chanzo | Idadi ya Miti |
|---|---|---|
| 1. | Ujazo wa Juu | Miti isiyo pungua 2 |
| 2. | Ujazo wa kati | Miti isiyo pungua 4 |
| 3. | Ujazo wa chini | Miti isiyo pungua 5 |

JEDWALI LA SABA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 37(1))*

KIBALI CHA KUTUMIA ENEO LA UTALII

Kibali hiki kimetolewa kwa Bw/Bi:…………………………….…………………………….……wa S.L.P……………….,Dar es Salaam. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ameridhia Ndugu mtajwa hapo juu, kutumia eneo la utalii lililopo…………………Mtaa wa………………………Kata ya ………………… baada ya kulipia ada ya kibali.

Mwombaji anaruhusiwa kufanya shughuli zifuatazo:
………………………………………………….………………………………………………
….…………………………………………………………..………………………………………
………………………………………..katika eneo hilo kuanzia tarehe…………Mwezi……………..Mwaka…………….mpaka
tarehe…….Mwezi……Mwaka……

<u>TAMKO LA MWOMBAJI;</u>
MIMI………………………………………………………nipo tayari kufuata masharti ya kibali hiki cha kutumia eneo la utalii na ninathibitisha kwa hiari yangu nimeelewa vema masharti ya kibali hiki.

Jina: ………………………Saini …………………..Tarehe …………………

*<u>KWA MATUMIZI YA OFISI;</u>*

Mwombaji amelipia Shilingi…….tarehe………mwezi……..Mwaka………….
(Ambatanisha stakabadhi ya malipo na fomu hii)

Jina la Afisa aliyetoa kibali……………… Saini …………… Tarehe ………….
Muhuri:…………………………………………….

JEDWALI LA NANE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 39)*

ADA ZA KUTUMIA MAENEO YA UTALII

| Namba | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Tozo ya ukitaji wa mahema ndani ya eneo la Hifadhi kwa siku kwa hema moja | 10,000.00 |
| 2. | Tozo ya kutumia mitumbwi, baiskeli, pikipiki, ndege ndogo, farasi na ngamia ndani ya msitu kwa masaa matatu kwa siku | 5,000.00 |
| 3. | Tozo ya uvuvi wa kimichezo kwa kila samaki | 20,000.00 |
| 4. | Tozo ya kupiga picha kwa maharusi | 20,000.00 |

*Tangazo la serikali Na.1011 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5. | Tozo ya kukita mahema kwa maharusi kwa siku. | | 30,000.00 | |
| 6. | Tozo ya uhifadhi kwa wanaolala katika eneo la Hifadhi kwa uhitaji wa mahema au nyumba za wageni | | 5,000.00 | |
| 7. | Tozo ya ukodishaji wa pikipiki ya tairi tatu katika utalii wa ndani katikati ya Jiji kwa safari | | 30,000.00 (kwa watanzania) | |
| | | | 50,000.00 (kwa raia wa kigeni) | |
| 8. | Tozo ya ukodishaji wa Basi kwa safari kwa kikundi | | Gharama ya mafuta jumlisha asilimia 70 ya gharama ya mafuta kwa watanzania | |
| | | | Gharama ya mafuta jumlisha asilimia 90 ya gharama ya mafuta kwa raia wa kigeni | |
| 9. | Tozo ya kuongoza safari za wageni kwenye vivutio vilivyopo Jiji la Dar es Salaam kwa safari. | | 20,000.00 kwa Watanzania | |
| | | | Dola za Kimarekani 20.00 Kwa raia wa kigeni | |
| 10. | Tozo ya kiingilio kwenye maeneo ya vivutio vya utalii | | kwa watanzania (Shilingi) | kwa raia wa kigeni(Dola za Kimarekani) |
| | (a) | Umri chini ya miaka 5 | Bure | Bure |
| | (b) | Umri kati ya miaka 5 na 15 | 1,000.00 | 5.00 |
| | (c) | Umri wa miaka 16 na zaidi | 3,000.00 | 10.00 |
| 11. | Tozo nyinginezo | | | |
| | (a) | Tozo za tafiti (Bench fee) | 40,000.00 | 50.00 |
| | (b) | Tozo za upigaji picha za mnato | 20,000.00 | 20.00 |
| | (c) | Tozo za upigaji picha mjongeo | 30,000.00 | 40.00 |
| | (d) | Tozo za kufanya tamasha/tukio | 50,000.00 | 100.00 |
| 12. | Ada ya kudhinisha kibali cha Nyara | | 10,000 | 20,000 |
| 13. | Ada ya kuidhinishiwa kibali cha mazao ya nyuki | | 5,000 | |

______________

JEDWALI LA TISA

______________

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 43)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi…………………………………..………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji La Dar es Salaam, kwamba mnamo tarehe…… ya mwezi…………….…..Mwaka ……….. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …………… ya Sheria Ndogo ya (Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji La Dar es Salaam. niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo Tarehe…ya Mwezi……………Mwaka…….

Jina…………………………………..…..

Saini………………………………...….

Mbele ya:

Jina………………………………………….

wadhifa………………………………………

Saini……..…………………………………..

Tarehe: ……………………………………..

*Tangazo la serikali Na.1011 (Linaendelea.)*

Lakiri ya Jiji la Dar es Salaam imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutao wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam uliofanyika tarehe 6/3/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

JOMAARY MRISHO SATURA,
*Mkurugenzi wa Jiji,*
*Halmashauri ya jiji,*
*Dar es salaam*

MHE. OMARY KUMBILAMOTO,
*Msahiki meya,*
*Halmashauri ya jiji,*
*Dar es salaam*

**L.S**

**NAKUBALI**,

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*

Dodoma,
29 Agosti, 2024